اللغة السواحلية

Kiswahili

# DALILI YA MUISLAM MPYA

## Ni nini uislam?

Syaikh Dr. Haitsam Sarhan

دليل المسلم الجديد، ما هو الإسلام؟

للشيخ د. هيثم سرحان

رِسَالَةٌ مُخْتَصَرَةٌ بِعُنْوَانِ:

# «كَيْفَ أَدْخُلُ فِي الإِسْلاَمِ؟»

مُتَرْجَمَةٌ إِلَى اللُّغَةِ: السواحلية

# «Nitaingia katika uislamu aje?»


إِعْدَادُ الْفَقِيرِ إِلَى عَفْوِ رَبِّهِ:

## هَيْثَم بْنِ مُحَمَّدٍ سَرْحَان

الـمُدرِّس بمعهد الحرم بالمسجد النَّبويِّ -سابقًا- والـمُشرِف على معهد السُّنَّة

https://mahadsunnah.com/


غفر الله له ولوالديه ولمن أعانه على إخراج هذا الكتاب

قامَ بتَرجَمَتِها: ...................... -وفَّقَهُ اللهُ وسَدَّدَهُ-


الطَّبعة الأولى



[حقوق الطَّبع مُتاحةٌ لكلِّ مسلمٍ بدون أيِّ تغييرٍ في المُحتوى]

¢

| Swali: | Jawabu: |
|---|---|
| Je kuingia katika dini ya kiislamu ni rahisi? | Ndio, haihitaji mtu wa katikati wala sherehe. |
| Je niharakishe kuingia katika uislamu au ningoje wakati inayofaa au baada ya kumaliza shida zingine? | Ni lazima ufanye haraka؛ kwa sababu kuchelewesha kuingia katika uislamu inaeza leta shida؛ unaeza kufa wakati wowote، kama vile kuingia katika uislamu ni Biashara iliyo nzuri, ukiingia haraka faida pia itakuwa kubwa. |

| Swali: | Jawabu: |
|---|---|
| Mwenye anataka kuingia katika uislamu Atafanya nini? | Anahitaji kusema tu shahada mbili:(nashuhudia ya kuwa hakuna apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah na nashuhudia mtume صلى الله عليه وسلم ni mja wake na mtume.) |
| Katika lugha gani yafaa mtu kusema shahada? | Anaeza sema na lugha yoyote ambaye anajua na si lazima iwe katika lugha ya kiarabu. |
| Anasema bila ya kujua maana yake? | La,Bali lazima ajue maana yake na afahamu itikadi yake na afanyie kazi. |
| Ni nini maana ya (nashuhudia?) | Maana yake ni nakiri na natambua na moyo wangu na |

| Swali: | Jawabu: |
|---|---|
| | nasema na ulimi na nafanyia kazi na sehemu zangu za mwili. |
| Nini maana ya «لَا إِلَهَ إِلَّا الله»? | Maana yake:Hakuna apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah. |
| Nini maana ya : (Muhammad ni mja na mtume? ) | Maanaa yake: Ni mja ambaye haabudiwi, na ni mtume haongei uwongo, na inamlazimu anayesema hii shahada aamini aliyosema mtume, afuate amri yake, awache aliyokataza, afuate sunnah yake, na mwenendo wake. |

| Swali: | Jawabu: |
| --- | --- |
| Nimefahamu vizuri, sasa napaswa kufanya nini? | Sema na mimi:(Ashhadu ala illaha ila Allah, wa ashhadu Anna Muhammadan abduhu wa rasuluhu.) |
| Je mimi sa hii ni Muislamu? | Ndio, AlhamdullillaAllah hii ni fadla ya Allah kwako. |
| Ni wasia gani unanipa sasa kama muislamu? | Nakupa wasia uombe Allah akuthibiti katika dini yake, na uchague warafiki wema watakaokusadia kuabudu yeye na uijifunze dini yako na ufiche uislamu wako mpaka iwe na nguvu kwa uwezo wa Allah. |
| Ni dua ipi iliyo bora zaidi? | (Tuongoze njia liyo nyooka.) Suratul fatiha ayah 6 |

| Swali: | Jawabu: |
| --- | --- |
| Ni dhikr gani iliyo kuwa rahisi sana? | Dhikr iliyokuwa rahisi ni (BismiAllah), inasemwa ukiingia msikiti na ukitoka, ukiingia nyumbani na ukitoka,ukisoma Quran, kabla ya kuingia choo, kabla ya kutoa nguo, kabla ya kutawadha, kabla ya kukunywa na kukula na zinginezo. |
| Ni nini hukmu ya madhambi niliyofanya kabla kuingia katika uislamu? | Uislamu inafuta dhambi zote ulikuwa nazo isipokuwa kama ni haki ya binadamu unafaa kumrudishia haki yake. |

| Swali: | Jawabu: |
|---|---|
| Nini napaswa kufanya baada ya kusema shahada? | Yafaa uoge. |
| Kwa nini naoga? | **<u>Kwanza:</u>** Muislamu hasemi kwa nini? anasema(tumesikia na tumetii) Suratul nur ayah 51<br>**<u>Ya pili:</u>** Unaoga ili usafishe mwili wako kama vile umesafisha ndani ya mwili yako. |
| Sawa, nitaoga aje? | Kwa kuweka nia kwa moyo yako unataka kuoga, halafu unasema (BismilAllah) na unaoga mwili wako wote na maji. |
| Baada ya kuoga nifanye nini? | ikifika wakati wa kusali, unasali kwa uwezo wa Allah. |

| Swali: | Jawabu: |
| --- | --- |
| Salah ni ngumu kwangu kwa sababu kuna vitendo na maneno ambayo ni ngumu? | Uislamu ni dini nyepesi, na sio dini ngumu, na shukrani zote ni kwa Allah. |
| Nitasali aje? | Ni lazima ufuate salah pamoja na mimi, au uangalie video ya kufundisha vile ya kusali, na utapata video katika lugha tofauti katika kituo cha mahad sunnah ambaye tovuti iko mwisho wa hii risala. |
| Halafu baada ya salah? | Lazima ujifundishe nguzo tano za uislamu halafu nguzo za imani ukiendelea.....mpaka ukamilishe |

| Swali: | Jawabu: |
|---|---|
| | kila kitu itafanya imani yako na uislamu iwe sahihi. |
| Ni tovuti gani utanipa nasiha nijifundishe uislamu? | Nakunasihi tovuti ya ma ulamaa waliokuwa na elimu, na waliopata elimu kutoka nchi ya Saudi Arabia. |
| Kivipi nitaamiliana na familia yangu wasiokuwa waislamu? | Utaamiliana na hao kama vile mtume صلى الله عليه وسلم aliamiliana na wasiokuwa waislamu, alikuwa akiita watu katika uislamu na ulimi wake na tabia yake na vile aliamiliana na watu. |

| Swali: | Jawabu: |
|---|---|
| Kuna yule anataka kuingia katika uislamu lakini hataki kuambia familia yake, hukmu yake ni nini? | Sio lazima aliyekuwa muislamu aambie mtu yeyote, uislamu yake ni baina yake na Allah. |
| Ni kitabu gani bora katika uislamu? | Kitabu bora ni Qurani Tukufu, ni maneno ya Allah. |
| Ni surah gani muhimu katika Qurani Tukufu? | Surah muhimu ni Al fatiha, kwa ajili ya hii, tunaisoma katika kila rakaa. |
| Ni ayah gani bora katika Qurani Tukufu? | Ayah bora katika Qurani Tukufu ni ayatul kursi. |

| Swali: | Jawabu: |
|---|---|
| Nitasoma Quran aje? | Kwa kujifundisha, na kuisikia ikisomwa, kama vile kusikiza sheikh Hudheify na Husary na wengine. |
| Nitafahamu Quran vipi? | Utafahamu kwa kusoma vitabu za tafsir iliyoandikwa na ma ulamaa walioshuhudiwa na ummah. |
| Nitapata wapi tafsir ya Quran? | Nakunasihi kwa mahala ambapo mushaf zinachapishwa nakala huko Madina. |
| Unani nasihi nisome nini baada ya Quran? | Nakunasihi usome hadith za mtume صلى الله عليه وسلم zilizokuwa sahihi. |

| Swali: | Jawabu: |
|---|---|
| Ni kitabu gani bora ya hadith? | Kitabu bora ya hadith na iliyo sahihi kabisa ni (sahih al-bukhari) Ummah umeafikiana kwa hilo,na ulamaa wameridhia hiyo, na nakunasihi kupakua vitabu katika mwisho wa hii risala kwa tovuti ilioyokuwa hapo chini. |
| Ni hadith gani muhimu sana katika sunnah? | Ni hadith ya Jibril inayobainisha viwango vya dini: uislamu, imani, ihsan. |
| Mimi nahofia ya kuwa sitajifundisha uislamu? | Usiogope bali tegemea Allah, Allah Akurahisishie, dini ni nyepesi, Allah akuafikishe kwa Alilopenda na Kuridhia. |

| Swali: | Jawabu: |
|---|---|
| | na unaweza pia kusoma na sisi bila malipo katika mahad sunnah kwa kufuata tovuti mwisho mwa hii risala.<br><br>Kumalizia, nakunasihi na hadith ya mtume صلى الله عليه وسلم.( **fanya bidii kutafuta itakayo kufaidi, mtegeme Allah, na usichoke.)**<br><br>سواحلي 🇰🇪 **kwa kiswahili - Uislamu-maahad ya sunnah. Inasimamiwa na:Dr. Haytham sarhaan.** |

| Swali: | Jawabu: |
| --- | --- |
| | اللغة السواحلية<br><br>kiswahili<br><br>YouTube<br><br>https://www.youtube.com/channel/UCl_5elx1FK7yGrPPFC1KGjw<br><br>https://youtube.com/@swahilisunnahinstitute<br><br>https://youtube.com/playlist?list=PLBFEt29we81RSyzi41l8uf1tvXvDO4n9e |

| Swali: | Jawabu: |
|---|---|
| | Facebook<br><br>https://www.facebook.com/pg/43-%D8%B3%D9%88%D8%A7%D8%AD%D9%84%D9%8A-D-Haythem-sarhan-113908833334500/community/<br><br>Telegram<br><br>https://t.me/hsarhan41<br><br>https://whatsapp.com/channel/0029VaDHYraEVccKt5Y7Sv1k |

| Swali: | Jawabu: |
| --- | --- |
| | 📚https://sarhaan.com/a/swahili-kiswahili-%d8%a7%d9%84%d8%b3%d9%88%d8%a7%d8%ad%d9%84%d9%8a%d8%a9/ <br><br> Site <br><br> https://alsarhaan.com/swa <br><br> Asalamu aleykum warahmatullahi wabarakatu. Kwa fadla ya Allah hii ndo kituo chetu mpya kwa lugha ya kiswahili <br><br> https://www.youtube.com/chan |

| Swali: | Jawabu: |
| --- | --- |
| | nel/UCVjvT26ZoWWPs49Xu6oS_Ag<br><br>Iko tayari kwa ukaguzi, Je munaweza kutusaidia kukagua na kutuma maoni.<br><br>Na pia kushiriki katika kituo na kutuma katika Vikundi.<br><br>Allah ajalie iwe katika mizani yenu. |

KISWAHILI سواحلي

# 3 VIGAWANYO VYA TAWHIID

Kumpwekesha Allah aliyetukuka kwa yale yanoyomuhusu yeye katika ulezi na uungu, na majina na sifa.

**Aina zake ni tatu**

### Tawhiid ya majina na sifa

Ni kumpwekesha Allah kwa alivyojiita na kuisifu nafsi yake katika kitabu chake au kupitia ulimi wa mtume wake ﷺ kwa kuthibitisha ya aliyoyathibitisha kwa ajili ya nafsi yake na kupinga yale aliyoyapinga kwa nafsi yake pasi na kupindisha au kukanusha au kuweka namna na kufananisha.

### Tawhiid ya uungu

Ni kumpwekesha Allah kwa ibada au kwa matendo ya waja

### Tawhiid ya ulezi

Ni kumpwekesha Allah kwa vitendo vyake au kumpwekesha kwa kuumba na ufalme na kupangilia mambo.

# Daraja za dini ni tatu

### Ihsaan

Ni kumuabudu ALLAH kama unamuona ukiwa humuoni basi yeye anakuona.

**Nguzo moja chini yake kuna daraja mbili**

1- Ibada ya mushaahada ni kumuabudu Allah kama unamuona.

2- Ibada ya muraaqaba ukiwa humuoni basi yeye anakuona.

### Imani

Ni kusema kwa ulimi na kuiakidi kwa moyo na kufanya matendo kwa viungo kunazidi, inapanda na inashuka.

**Nguzo za imani 6**

1- Kumuamini Allah
2- Na Malaika wake
3- Na vitabu vyake
4- Na mitume yake
5- Na siku ya mwisho
6- Na kuamini qadari kheri zake na shari zake.

### Uislamu

Ni kujisalimisha kwa Allah aliyetukuka kwa kumpwekesha na kunyenyekea kwake kwa kumtii na kujitenga kutokna na shirki na watu wake

**Nguzo za uislam 5**

1- Shahaa mbili
2- Kusimamisha swala
3- Kutoa zaka
4- Kufunga Ramadhani
5- Kuhiji katika nyumba ya Allah kwa mwenye kuweza kuiendea

# 4 Vigawanyo vya mambo ya haramu

### Dhambi ndogo

(zilizo chini ya dhambi kubwa) dhambi kubwa hufutwa kwa istighfaar Na dhambi ndogo inakua kubwa kwa kudumu amesema mtume ﷺ jiepusheni na madhambi madogo kwani hukusanyika kwa mtu mpaka yanamuangamiza)

### Dhambi kubwa

( Kila dhambi iliyoekewa adhabu maalumu) kama uchawi, kuwaasi wazazi, riba, zina,liwati, uongo, kunywa pombe, kuiba, kusengenya,kuua nafsi aliyoiharamisha Allaah isipokua kwa haki,kula mali ya yatima.

### Shirki ndogo

(Haitoi kwenye dini ni dhambi kubwa kuliko madhambi makubwa)Kama kusema ametaka Allah na umetaka wewe, kuapa kwa asiekua Allah, kujionesha , hirizi za shirki, kuitakidi nukhsi, kutungika viganja na shangan a mfano wake kwa ajili ya kutaka hifadhi na kuondosha vijicho.

### Shirki kubwa

(Ni yenye kutoa katika dini hasamehewi mtu akifa nayo) Kumjaalia Allah mshirika anamuomba kama anavyomuomba Allah au anamuogopa au kumtarajia au kumpenda kama anavyompenda Allah au anamfanyia aina katika aina za ibada.

# Sifa ya udhu na tayammum na kuoga

2

## Sifa ya udhu

Atanuia udhu kwa moyo wake kisha atasema bismillah kisha ataosha viganja vyake.



1

Kisha atachukua maji kwa kiganja chake cha kulia na atasukutua na kupandisha maji puani na kuyameka na ataweka kidole gumba na cha ishara puani.



2

Kisha ataosha uso wake kutokea maoteo ya kawaida ya nywele za kichwa mpaka mwisho wa taya mbili na kidevu kwa urefu na upana baina ya maskio mawili.



3

Kisha ataosha mikono yake kutokea ncha za vidole mpaka katika viwiko ataanza mkono wa kulia kisha kushoto.



4

Kisha atapatangusa kichwa chake chote atapitisha mikono yake kutokea mwanzo wa kichwa mpaka kisogoni kisha atarejesha mwanzo wa kichwa.



5

Kisha ataingiza kidole chake cha ishara katika tundu za maskio yake na atapakaa kwa kidole gumba nje ya masikio.



6

Kisha ataosha miguu yake pamoja na fundo mbili.



7

- Hukumu ya kuzidisha juu ya kiwango kilichoekewa sheria ?

Haifai kuzidisha juu ya kiwango kilichoekewa sheria katika udhu kama kuzidisha kuosha mara tatu au kuosha juu ya kiwiko au juu ya fundo za miguu (miundi) au kupaka shingo.



8

- Na atasema baada ya kumaliza kutia udhu :

“Ash hadu alla ilaaha illa Allaah wahdahu laa shariika lahu wa ash hadu anna muhammadan 'abduhu wa rasuuluh” na katika mapokezi ya tirmidhi “Allaahumma j'alnii mina ttawwaabiin waj'alnii minal mutatwahhiriin”

9

- Miongoni mwa vitenguzi vya udhu :

1- Chenye kutoka tupu ya mbele na nyuma kama mkojo au haja kubwa au upepo.
2- Kutokwa na akili kwa kulala au kuzimia.
3- Kula nyama ya ngamia.

10

## Sifa ya tayammum

Tayammum ni badali ya twahara ya maji itakaposhindikana kutumia maji katika viungo vya twahara au baadhi yake kwa sababu ya kukosekana maji au kuhofia madhara kwa kutumia maji, basi ytachukua mchanga nafasi ya maji

1

Atanuia tayammum kwa moyo wake kisha atasema bismillah kisha atapiga pigo moja juu ya ardhi na atapangusa kwa viganja vyake uso wake na nje ya viganja vyake.




2

wala si sheria kuchanua vidole wakati wa kupiga juu ya mchanga wala kuesua vidole wakati wa kupangusa viganja viwili



3

## Sifa ya josho la wajib

Atanuia kuoga kwa moyo wake na atasema bismillah
Kwa siri kisha ataeneza mwili wote kwa maji na sehemu zilizo chini ya nywele chache na nyingi pamoja na kuskutua na kupandisha maji puani.

1

- Yenye kuwajibisha kuoga :

1- Janaba: inakuwa kwa kutoa manii kwa kuingilia au jambo jengine au kukutana kwa tupu mbili. 2- kutoka damu ya hedhi na nifasi. 3- Kifo cha asiekuwa shahiid 4- Kusilimu kwa kafiri

2

Ameweka taaliki Sheikh Duktuur Haytham Sarhaan , Mwalim wa zamani masjid annabawiy
Na msimamizi wa maahad ya sunna : mahadusunnah.com

Haki za kuchapa na kusambaza zipo huru.
Tarjama ya kipeperushi «sarhaan.com» Au pangusa bar code

# Sifa ya swala ya mtume ﷺ

1

Ni sunna kwa imam na mwenye kuswali peke yake aswali kuelekea sutra.
Na sutra ya imaam ni sutra ya aliye nyuma yake.

Na atajaalia macho yake sehemu anayosujudia, wala asigeuke geuke.



1

Na atajaalia umbali wa nyayo ylzake kama umbali wa mabega yake hatozidisha wala kupunguza na ataweka sawa miguu yake.



2

Baada ya kuleta sharti za swala atasema "Allaahu akbar" pamoja na kunyanyua mikono hali ya kubandanisha vidole usawa wa masikio au mabega na atajaalia ndani ya viganja kuelekea qibla.



3

Kisha ataeka kiganja chake cha kulia juu ya nje ya kiganja na mkono wa kushoto juu ya kifua chake.



4

Kisha ni sunna kusoma dua ya kufungulia swala katikavrakaa ya kwanza tu na ni bora afanye aina tifauti tofauti za kufungulia swala na atasema " Subhaanaka Allaahumma wa bihamdik wa tabaaraka ismuk wa ta'ala jadduka wa laa ilaaha ghayruk.

Kisha atasema "A'uudhu billaahi mi shaytwaani rrajiim"

Kisha Atasoma bismillaahi na atasoma suuratul faatiha kama ilivyopangiliwa kwa aya zake na maneno yake na herufi zake na haraka zake.
Bismillahi rrahmani rrahiim(1)
Alhamdu lillaahi rabbil aalaamiin (2) Arrahmaani rrahiim (3) Maaliki yawmi ddiin (4) Iyyaaka na'budu wa iyyaaka nasta'iin (5) Ihdina sswiraatwa Imustaqiim (6) swiraatwa Iladhiina an'amta 'alayhim ghayril maghdhwuubi 'alayhim wala dhwaalliin (7)

Kisha atasoma kinamwepesikia katika Qur'an (sunna) bila ya kuleta isti'aadha na atasoma bismillaahi mwanzi wa sura tu.

5

Kisha atanyanyua mikono yake kama alivyonyanyua katika takbira ya kuhirimia swala hali ya kusema "Allaahu akbar" na atarukuu kisha atakamata magoti yake na wala hatokunja viwiko vyake na atafanya mgongo wake kuwa sawa na kichwa chake na atasema mara moja kwa uwajibu "subhaana rabbiyal 'adhwiim" na ni sunna kuzidisha kwa yaliyothibiti.



6

Kisha wakati wa kunyanyuka na kabla ya i'tidaal atasema "sami'a Llaahu liman hamidah" pamoja na kunyanyua mikono yake usawa wa masikio yake au mabega yake.

Atakaponyooka wima atasema "Rabbanaa wa laka lhamd" na ni sunna kuzidisha dua zilizothihiti

Kisha ataleta takbira bila ya kunyanyua mikono na atasujudu juu ya viungo saba : paji la uso, pua na viganja viwili na magoti mawili na matumbo ya vidole vya miguu.

Na ataweka umbali baina ya makwapa na baina ya tumbo na mapaja na baina ya mapaja na miundi navatanyanyua dhiraa zake.



7

Na atasema "subhaana rabbiyal a'laa" mara moja wajibu na atazidisha kwa zilizothibiti katika adhkaar na inafaa aombe anachotaka na bora aombe kwa dua zilizothibiti.



8

Kisha atatoa takbira na atakalia mguu wake wa kushoto hali ya kuwa ameutandaza na ataunyanyua wa kulia na ataweka matumbo ya vidole vya kulia ardhini na vidole vyake kuelekea qibla, na ataweka viganja vyake kuu ya mapaja yake na atasema "Rabbi ghfirliy". Hiki kikazi ni katika vikazo vyite vya swala isipokuwa katika swala ya rakaa 3 na 4 katika tashahhud ya mwisho atakaa "tawarruk" kwa kufanya mguu wake wa kushoto chini ya muundi wa kulia.



9

Kisha atatoa takbira na atasujudu kama sijda ya kwanza kisha atatoa takbira na atasimama kwa ajili ya rakaa ya pili na atafanya kama alivyofanya katika rakaa ya kwanza isipokuwa katika rakaa ya pili hakuna takbira ya kuhirimia na dua ya kufungulia swala.



Atakapomaliza sijda ya pili atakaa kwa ajili ya tashahhud.

Na ataashiria kwa kidole chake cha ishara na atazungusha duara kidole cha kati na gumba, na atatikisa kidole cha ishara na kuomba.



Na atasoma tashahhud kisha swalaatul ibraahimiyya "Attahiyyaatu lillahi waswalawatu wa twayyibaatu assalaamu 'alayka ayyuha nnabiyyu warahmatullah wabarakaatuh assalaamu 'alaynaa wa 'alaa 'ibaadi llaahi swaalihiin ash hadu an la ilaaha illa llah wa ash hadu anna muhammadan 'abduhu warasuuluh Allahumma swalli alaa muhammad wa 'alaa aali muhammad kama swallayta 'alaa ibrahim wa 'alaa aali ibrahim innaka hamiidun majiid Allaahumma baarik alaa muhammad wa 'alaa aali muhammad kama baarakta 'alaa ibrahim wa 'alaa aali ibrahim innaka hamiidun majiid.

Kisha ataomba kinga kutokana na mambo manne "Allaahumma inni a'udhubika min 'adhaabi jahannam wa a'udhubika min 'adhaabil qabr wa a'udhubika min fitnatil mahyaavwal mamaat" na ataomba anachokitaka na bora aombe kwa yale yaliyothibititi pamoja na kusema "Allaahumma a'inni 'alaa dhikrika wa shukrika wa hisni 'ibaadatik"

Kisha atatoa salamu mbili kulia na kushotoni kwake hali ya kusema "Assalaamu 'alaykum wavrahmatullaah" na atageuka kwa kichwa chake tu bila ya mabega na bila ya kutikisa kichwa juu na chini na bila ya kuashiria kwa mikono .



10

Ameweka taaliki Sheikh Duktuur Haytham Sarhaan , Mwalim wa zamani masjid annabawiy

Na msimamizi wa maahad ya sunna : mahadusunnah.com

Haki za kuchapa na kusambaza zipo huru.
Tarjama ya kipeperushi «sarhaan.com» Au pangusa bar code

# (DALILI YA UTUME).

# AL QURANI TUKUFU.

Yahya ibn Aktham alisema: Al-Mamun,ambaye alikuwa kiongozi wakati huo, alikuwa na kikao cha mjadala, akaingia miongoni mwa watu kijana myahudi, ambaye alikuwa na nguo nzuri na alikuwa akipendeza na pia alikuwa na manukato nzuri na akaongea kwa ufasaha.

Wakati kikao iliisha, Al-Mamun akamwita akamwuliza wewe ni myahudi?

Akasema : Ndio

Al-Mamun akamwambia: Kuwa mwislamu na nita kupatia vitu nzuri kadha wa kadha– na akamwahidi vitu nzuri ikiwa ataingia katika dini ya uislamu.

Myahudi akajibu: Bali nitakaa na dini yangu, dini ya babu zangu halafu akaondoka ile kikao.

Baada ya mwaka, yule Myahudi akakuja – na alikuwa mwislamu. Akaanza kuongea kuhusu fiqh na Hadith – na akaongea kwa ufasaha.

Baada ya kikao kuisha, Al-Mamun akamwita akamwuliza: Si wewe ni yule Myahudi tuliye mwona ile siku?

Akasema: naam.

Al-Mamun akamwuliza: Mbona umekuwa muislamu?

Myahudi akamwambia: Sikiza, na useme “Allahu Akhbar”

Ile siku wakati nilitoka kikao chako, nilitaka kupatia mtihani hizi dini tofauti – na mimi ni mhodari wa kuandika. Nikachukua nakala ya Torah na nikaandika nakala tatu zingine lakini nikaongeza vitu na nikatoa zingine. Nikazipeleka kwa hekalu la kiyahudi , wakazinunua kutoka kwangu na hawakuzisoma wala hawakuzipitia. Nikachukua nakala ya bibilia, nikaandika nakala tatu zingine lakini nikaongeza vitu na nikatoa zingine . Nikazipeleka kanisa, wakazinunua kutoka kwangu lakini hao pia hawakuzisoma wala hawakuzipitia.

Kisha Nikachukua nakala ya Qur’an, nikaandika nakala zingine tatu lakini nikaongeza vitu na nikatoa vitu zingine.Nikazipeleka kwa waandishi wa kiislamu wakasema hatutazikubali mpaka tuzipitie na tuziangalie . Wakati waligundua zile makosa - vitu nilizoongeza na zile nilitoa, walichoma zile vitabu na karibu waniue. Kwa hivo, nikajua hii Kitabu(Qur’an) ni kitabu iliyohifadhiwa na Allah – hii ndo sababu ya mimi kukuwa mwislamu.

# Zakah ni Aina mbili

**Sunnah: ile ambaye mtu anatoa kwa kujikaribisha kwa Allah**

**Wajib:**

**Ni Aina mbili:**

## Zakah ya mwili:

zakaatul fitr ambaye ni wajib kwa kila muislamu, mkubwa na Mdogo, mvulana na msichana, mtumwa na huru.

## Zakah ya Mali.

Ni kuabudu Allah kwa kutoa kiwango ambaye ni wajib kisheria kwa Mali ambaye ni maalum kwa watu au njia zinazofaa. Ni nguzo tatu ya uislamu.

Iko viwango vinne:

**1 Pesa**



dhahabu na fedha na sarufi.
Nisab ya dhahabu (85g)
Nisab ya fedha (595g)

**2 Wanyama wa kuchunga**



inayokula zaidi ya mwaka au yote. Hawa ni ngamia, Ngombe na mbuzi.

**3 Vinavyotoka katika ardi:**



ngano na matunda

**4**



Vitu vya kufanya Biashara nazo.

# Watu wa kupewa zakah

**1 Fukara:** ni watu waliokuwa na haja na hawa a chochote au wako na kitu kidogo.

**2 Masakin:** ni watu ambao wako na mahitaji yao au nusu ya mahitaji yao, tukiweka mahitaji ya mwaka iwe elfu kumi na mbili, fakiri ni yule ako na elfu sita au hana kitu, na maskini ni yule ako na elfu sita au zaidi lakini hajafikisha elfu kumi na mbili, kwa sababu tunapatia maskini na fukara kitu ambacho inawasaidia kwa mwaka mzima kwa kuwa zakah inakuwa wajib kwa mwaka.

**3 Wanaofanya kazi ya kuchukua zakah** Ni waliowakilishwa kugawa zakah, wanachagulia na kiongozi wa waislamu, sio lazima wawe fakiri, Bali wanapewa zakah hata kama ni matajiri.

**4** Wale ambao wanatarajiwa kuwa waislamu au kuzuia shari zao au wanaopewa ili imani yao iongezeke.

**5 Watekwa nyara, nao ni:**
1. Muislamu aliye andikiwa mkataba ya kuwachwa huru.
2. Kuweka huru muislamu aliyetekwa nyara.
3. Muislamu aliyetekwa nyara.

**6 Waliokuwa na deni:**
1. Waliokuwa na deni kuleta suluhu baina ya watu.
2. Aliokuwa na deni.

**7 Wanaofanya jihad kwa ajili ya Allah,** na vitu wanazozihitaji kama silaha na zinginezo.

**8 Msafiri aliyeishiwa** Msafiri aliyeishiwa na pesa yake kwa safari yake, anapewa kiwango ya kumfikisha nchi yake.

# Saum ni Aina mbili

**Sunnah:** ni saum Zisizokuwa za wajib.

**Wajib:** kama vile ramadhan na saum ya kafara na saum ya kuapa.

**Maana ya saum**

Ni kuabudu Allah kwa kujizuia kukula na kukunywa na kukaa mbali na vitu zote zinazovunja saum kutoka fajr mpaka jua Itue.

## Saum iko na nguzo mbili

### 1 Nia

| Nia ya saum ya sunnah | Nia ya saum ya wajib |
|---|---|
| Inasihi kuweka nia wakati wowote wa mchana maadamu haja fanya vitu zinazovunja saum Lakini thawabu inaanza wakati wa kuweka nia. | Katika saum ya wajib ni lazima kuweka nia usiku yaani Kabla ya fajr. Na inatosheleza kuweka nia wakati mwezi wa ramadhan imeingia. Na mahala pa kuweka Nia ni moyo na kuisema na mdomo ni bid'a. |

### 2 kukaa mbali na vitu zinazovunja saum



**Vitu zinazovunja saum**

1-kukula na kukunywa kwa kusudi, atakayesahau saum yake ni sahihi 2-kufanya kitendo cha ndoa. Kama ni Mchana katika saum ya wajib anafaa alete kafara.
3-Kutoa mani. 4-Zilizokuwa mfano wa vyakula na vinywaji kama vile sindano iliyokuwa na chakula. 5-Kutoa damu kwa njia ya hijama.
6-Kujilazimisha kutapika
7. Kutokwa na damu ya hedhi au nifaas.

**Vitu zilizoruhusiwa kwa aliyefunga.**

- Kuonja chakula kwa haja.
- Kumeza mate.
- Kufanya ghusl.
- Kutumia Mswaki.
- Kupaka manukato.
- Kuoga.

## Sharti zinazofanya saum iwe wajib

1. Kuwa muislamu
2. Kuwa na akili timamu
3. Kufika umri wa kubaleghe, ama asiyefika umri wa kubaleghe anahimizwa kufunga na anaamrishwa na wali wake.
4. Asiyekuwa msafiri. Saum si lazima kwa msafiri. Ni vizuri zaidi afunge saum kama hata pata uzito kulingana na kitendo ya mtume na kwa sababu ni rahisi kuliko kujiekea deni ya ramadhan na pia kutafuta fadla ya mwezi wa ramadhan.
5. Kukuwa na siha.
6. Kutokuwa na hedhi au nifaas

**Vitu ambazo ni haramu kufanya kwa aliyefunga:**

1. Kumeza kohozi lakini haivunji saum
2. Kupiga busu kwa asiyeweza kujimudu.
3. Kufanya uovu ambaye ni haramu.
4. Ujinga.
5. Kufunga saum mfululizo siku mbili bila ya kufuturu.

**Vitu zinazochukiza kufanya kwa aliyefunga**

1. Kuzidisha kwa kuweka maji kwa mdomo na mapua wakati wa kutawadha.
2. Kuonja chakula bila haja.




- **ARKAN YA HAJJ:** YEYOTE ATAKAE ACHA RUKN YA HAJJ, HAJJ HAIJATIMIA.
- **WAJIBAT YA HAJJ:** YEYOTE ATAKAE ACHA WAJIBAT YA HAJJ INAMLAZIMU KUCHINJA

alsarhaan.com
sarhaan.com

# Manasik ya Umrah

KISWAHILI سواحلي




## Vitu zinazokatazwa ukiwa katika hali ya ihram

1. Kutoa nywele katika kichwa au mwili
2. Kukata kucha
3. Kutumia manukato
4. Kujifanyia nikkah au mtu mwingine
5. Kufanya kitendo cha ndoa
6. Kuwinda wanyama wa ardi

**Vitu zilizokatazwa kwa wanaume peke yao**

1. Kuvaa nguo iliyoshoneshwa inayoshika mwili kama vile kanzu au katika sehemu yeyote ya viungo
2. Kuvaa kitu juu ya kichwa kama imamah au kofia

**Vitu ambazo zimekatazwa kwa wanawake peke yao**

1. Kufunika uso na niqab au burqa lakini akiwa mbele ya wanaume anafunika uso wake na khimar au kitu ingine.
2. Kuvaa kinga ya mkono.

## Vitu ambazo ni sunnah kufanya katika umrah:

1. Kukata kucha na nywele ambayo ni lazima Kuikata Kabla ya kuweka nia ya kuingia katika ihram
2. Kufanya ghusl ili kuingia katika ihram
3. Kupaka manukato kwa mwili na hii ni ya wanaume peke yao.
4. Kuvaa nguo nyeupe miwili kwa wanaume.
5. Talbiya, kusema (labaika Allahuma labaik labaika la sharika laka labaik innal hamda wa neemata laka wal Mulk la sharika lak.) Kuanzia wakati wa kuingia katika ihram mpaka afike katika tawaf.
6. Kuweka Bega la kulia wazi wakati wa tawaf na hii ni kwa wanaume peke yao.
7. Kubusu hajarul aswad.
8. Kukimbia kwa wepesi katika raundi tatu ya kwanza ya tawaf
9. Kusali rakaa mbili nyuma ya maqam Ibrahim.

As-Sunnah College

# Sunna za kimaumbile

**Sifa ambazo Allah amemuumba nazo mwanadamu.**

Mwanaadamu ana mahitaji ya msingi , japokuwa mazingira yanaweza kumuathiri . yametajwa mahitaji hayo ya msingi katika hadith za mtume zilizo sahihi.

| Sunnah | Hukmu | Maelezo |
|---|---|---|
| [1] Kupunguza sharubu. | Sunnah na inachukizwa kuzinyoa zote. | Sunnah katika sharubu ni kuzipunguza na kuzihafifisha hadi kudhihiri ncha za midomo. |
| [2] Kufuga ndevu | Wajibu | Ni haramu kunyoa ndevu kwa sababu n Kwenda kinyume na amri ya mtume ya kuzifuga. |
| [3] Mswaki | Sunnah iliosisitizwa | Kutumia mti wa "Araak" na mfano wake katika kusafisha meno ni sunna katika kila wakati na inahimizwa zaidi wakati wa udhu na wakati wa swala na wakati wakuingia nyumbani na msikitini na wakati wa kusoma Qur-an na kuamka kutoka usingizini na kwa aliyefikiwa na umauti na pindi inabobadilika harufu ya mdomo. |
| [4] Kupandisha maji puani | Katika sunnah za udhu | Kuosha pua kwa njia ya kuingiza maji puani na kuyatoa. |
| [5] Kukata kucha | Sunna wala haifai kuziacha zaidi ya siku 40. | Kukata kucha kwa sababu kuziacha ni sababu ya kukusanyika uchafu chini yake. |
| [6] Kuosha pingili za vidole | Sunnah | Kusafisha sehemu ambazo unakusanyika uchafu, nazo ni pingili za vidole. |
| [7] Kunyofoa nywele za kwapa | Sunna wala haifai kuziacha zaidi ya siku 40 | Kuondosha nywele zenye kuota kwapani sawasawa zimeondoshwa kwa kunyofoa au kunyoa au kwa njia nyengine, kwa sababu kuondosha kwake ni usafi na kukata harufu yenye kuchukiza. |
| [8] Kunyoa kinena | Sunna wala haifai kuziacha zaidi ya siku 40 | Nywele zenye kuota sehemu za siri.<br>Zinaweza kutolewa pasi na kuzinyoa, kama kutumia mafuta ya kisasa. |
| [9] Kustanji | Katika adabu za kukidhi haja. | Kuondosha vinavyotoka katika njia mbili kwa kuosha kwa maji na mfano wake katika sehemu inayotoka na zilizo karibu. |
| [10] Kusukutua | Katika sunna za udhu | Kuosha mdomo kwa njia ya kuingiza maji kisha kuyatoa. |

Kutoka kwa Aisha Allah amridhie amesema :Amesema mtume (ﷺ) : Mambo kumi ni katika fitrah: Kupunguza sharubu, Kufuga ndevu, kupiga mswaki, Kupandisha maji puani, kukata kucha, Kuosha pingili za vidole, kunyofoa nywele za kwapa, kunyoa kinena na kustanji. Amesema Zakariyya: Amesema Mus-ab nimesahau jambo la kumi , lakini inaweza kuwa kuskutua. (Imesimuliwa na muslim)

| | | |
|---|---|---|
| [11] kutahiri | Wajibu tkwa wanaume sunna kwa wanawake | Kukata ngozi inayofunika dhakar; ili usikusanyike uchafu ndani yake, na ili kutakasika na mkojo. |

Kutoka kwa Abu hurayra Allah amrdhie kutoka kwa mtume (ﷺ), amesema: "Mambo matano ni katika fitra: Kutahiri…" imesimuliwa na (Bukhari and Muslim)

Chanzo: Fathul Mu'een Fee Taqreeb Manhaj As-Saalikeen Wa Tawdheeh Al-Fiqh Fee Ad-Deen " Shaykh Haytham Sarhaan", chapa ya kwanza 1442 H

هيثم بن محمد سرحان

و لا تقف ما ليس لك به علم
Na wala usifuate usiyo na ujuzi nayo.

و اغضض من صوتك
na uishukishe chini sauti yako.

ادفع بالتي هي أحسن
uondoshe ubaya kwa wema.

و لا تنابزوا بالألقاب
wala msiitane majina ambayo mabaya

اجتنبوا كثيرا من الظن
Jiepusheni na dhana mbaya nyingi

و أطعموا البائس الفقير
Na mlisheni mwenye shida aliye fakiri.

و قولوا قولا سديدا
Na semeni maneno yanayolingana na usawa.

و احفظوا أيمانكم
Na chungeni viapo vyenu.

كونوا قوامين بالقسط
kuweni ni wasimamizi wa uadilifu.

و لا تلبسوا الحق بالباطل
Wala msichanganye haki na batili.

و اخفض جناحك للمؤمنين
na uwanyenyekee wenye kumuamini MwenyeziMungu na Mtume wake.

خذ العفو و أمر بالعرف
Shikamana na kusamehe na amrisha mema

و لا تأكلوا أموالكم بينكم بالباطل
Na wasile baadhi yenu mali ya wengine kwa njia ya batili

و لا تجسسوا
Wala msipelelezane

و بالوالدين إحسانا و ذي القربى و اليتامى
muwafanyie wema wazazi wawili na jamaa za karibu na mayatima

أنفقوا مما رزقناكم
Toeni miongoni mwa tulivyowaruzuku

و تعاونوا على البر و التقوى
Na saidianeni kufanya wema na kumcha Mwenyezi mungu

و زنوا بالقسطاس المستقيم
na mpime kwa mizani ya uadilifu iliyolingana sawa.

اعدلوا
Fanyeni uadilifu.

و لا تعثوا في الأرض مفسد
wala msitembee katika ardhi kuleta uharibifu.

و لا تصعر خدك للناس
Na usizungushe uso wako kwa kuwadharau watu.

و اعرض عن الجاهلين
na jiepushe na kushindana na wajinga wenye uchache wa akili.

لا تبطلوا صدقاتكم بالمن و الأذى
msiziondoe thawabu za vitu vile mlivyovitoa sadaka kwa usumbulizi na kero

و لا يغتب بعضكم بعضا
Wala msisengenyane myinyi kwa nyinyi

و إذا حييتم بتحية فحيوا بأحسن منها
Na Muislamu akiwatolea salamu, muitikieni salamu kwa maneno mazuri zaidi.

و آتوا اليتامى أموالهم
Na wapeni mayatima nali zao.

و لا تعاونوا على الإثم و العدوان
wala msisaidiane kwenye mambo ya madhambi, maasia na kuivuka mipaka.

و أوفوا الكيل إذا كلتم
Na timizeni kipimo wala msikipunguze mnapopima.

و لا تعتدوا
Wala msipite mipaka.

و لا تمش في الأرض مرحا
Na usitembee ardhini kwa kujigamba na kujivuna.

و اقصد في مشيك
Na unyenyekee katika kwenda kwako.

ادع إلى سبيل ربك بالحكمة
Lingania kwenye dini ya mola wako kwa kutumia hekima

لا يسخر قوم من قوم
Wasidharau kundi kulidharau kundi lengine

ادخلوا في السلم كافة
ingieni katika sheria zote za Uislamu.

و لا تتبدلوا الخبيث بالطيب
Walamsibadilishe kibaya kwa kizuri

و قولوا للناس حسنا
Na semeni na watu yaliyo mazuri.

و أوفوا بعهد الله إذا عاهدتم
Na jilazimisheni kutekeleza kila ahadi baina yenu nyinyi na Mwenyezi Mungu

بسم الله الرحمن الرحيم




# UFUPISHO WA KITABU ALWASAAILUL MUFIIDAH LIL HAYAAT ASSA'IYDAH

**MTUNZI:** Abdurrahman bin Nasir As-Si'di (1307 – 1376 H) Ni katika wanachuoni maarufu wa kiislamu na maimamu wahakiki.




**Sababu ya kutunga kitabu:** pindi aliposafiri sheikh kuelekea Lebanon kwa ajili ya matibabu mwaka 1373H alisoma kitabu "Acha wasiwasi na anza Maisha" cha mtunzi wa kimarekani Dale Carnagie akakipenda ndio akaamua atunge mfano wake kitabu hiki.




**(1) Kumuamini Allaah na kufanya matendo mema:** kwani Imani inapelekea katika subra na kuridhia na kukinai ulichopangiwa na Allah.




**(2) Kuwafanyia wema viumbe kwa kauli na matendo**: kwani kheri inaleta kheri nyengine na inaondoa shari.




**(3) Kujishughulisha na kazi au elimu yenye manufaa:** kwani kunaupumbaza moyo kufikiria yenye kutia wasiwasi.




**(4) Kuishughulisha fikra kwa kazi ya leo:** basi usihuzunike na yaliyopita wala usiwe nawasiwasi kuhusu yanayokuja kwani alikuwa mtume akijinga kwa Allah kutokana na wasiwasi na huzuni .




**(5) Kukithirisha kumtaja Allah aliyetukuka:** Kwani kumtaja Allah kunaleta utulivu wa moyo.




**(6) Kuhesabu neema za Allah za wazi na za siri:** kunaleta shukrani na kusahaulisha matatizo.



**(7) Kuwatazama walio chini yako:** kunapelekea katika kumshukuru Allah juu ya hali uliyonayo na kuondosha huzuni yako na wasiwasi wako.




**(8) Kusahau yaliyopita :** yaliyopita huwezi kuyarudisha na kujiishughulisha nayo ni upuuzi na wazimu.




**(9) Kumuomba Allah aliyetukuka:** kama kuomba akutengezee dini yako na dunia yako na akhera yako kama ilivyokujakatika hadith.




**(10) Kukadiria matokeo mabaya;** kwani pindi yakitokea mabaya yanakuwa hafifu , na yakitokea fanya juhudi kuyaondosha kwa kadri ya uwezo.




**(11) kutokithirisha kufikiria yasiyowezekana**; kwani huleta fikra mbaya na kupelekea kutokea mabaya , nayo ni sababu ya wasiwasi na maradhi.




**(12) Kuuegemeza moyo kwa Allah na kutegemea kwake**; na yeyote mwenye kumtegemea Allah basi yeye atamtosheleza.




**(13) Kuvumilia makosa ya wengine na kusubiri juu ya maudhi yao** ;kila mtu lazima awe na aibu au mapungufu au jambo unalochukia basi tazama upande wake mwengine ulio mzuri.




**(14) Usijishughulishe na mambo ya kipuuzi:** kama unavyoizoesha nafsi yako juu ya kuvumilia matatizo na mambo makubwa basi mambo madogo ni bora zaidi kuachana nayo.




**(15) Maisha mafupi:** Maisha ya uhakika- Pamoja na ufupi wake- ni Maisha ya furaha na kutulizana basi usiyafupishe zaidi kwa wasiwasi na kufikiria matatizo .




**(16) Wasiwasi mwingi hauna uhakika:** basi mambo mengi ambayo unapata waiwasi hayajatokea basi usiruhusu makadirio dhaifu kushinda makadirio mengi yenye nguvu.



**(17) Usikasirike kutokana na maudhi ya watu:** maudhi ya watu yanarejea juu yao ukishughulika nayo yatakudhuru kama yanavyowadhuru




**(18) Maisha yako yanafata fikra zako:**ikiwa fikra ni katika zile ambazo zinaleta manufaa juu yako katika dini au dunia basi Maisha yako ni ya furaha na kama sivyo basi ni kinyume.




**(19) Usisubiri shukrani kutoka kwa watu:** Ukifanya wema kwa yule mwenye haki juu yako au yule ambaye hana haki juu yako basi huo ni muamala wako Pamoja na Allah basi usijali kwa kutoshukuriwa.




**(20) Ishughulishe nafsi yako kwa yale yanayokunufaisha:** kwani mambo yenye kudhuru yanaleta wasiwasi na huzuni basi taka msaada kwa kufanya matendo yenye manufaa.




**(21) Fanya mambo kwa muda:** kwani mambo usipoyafanya kwa muda yatakusanyika mambo yaliyopita na yanayokuja kisha yatakushughulisha.




**(22) Pangilia mambo ya kufanya awali:** anza na jambo la muhimu zaidi kisha la muhimu na chagua lile ambalo nafsi yako ina egemea zaidi ili usipate uchovu na taka ushauri kwani hajutii mwenye kutaka ushauri.






# Ni nani Mtume Muhammad ﷺ, na kitu gani ametufundisha?

Ameweka taaliki Sheikh Duktuur Haytham Sarhaan

Mwalim wa zamani masjid annabawiy

Na msimamizi wa maahad ya sunna.

Au pangusa bar code - sarhaan.com

## Ni nani Mtume Muhammad ﷺ na kitu gani ametufundisha?

- Yeye ndio ametetea haki zote za viumbe tangu miaka 1400 ilopita.

- Amehifadhi haki za wanaume, wanawake, watoto na wanyonge.

- Amehifadhi haki za wanyama mimea na akahimiza kutunza mazingira.

- Ametuamrisha tabia njema na akapangilia mahusiano baina ya ndugu wa karibu na majirani.

-Na (akaasisi uhusiano) ya kuishi baina ya waislam na wasiokuwa waislam.

- Na akapangilia mahusiano ya kifamilia ambayo yanahifadhi haki kubwa za baba na mama kwa watoto wao.

## Ni nani Mtume Muhammad ﷺ na kitu gani ametufundisha?

- Amekataza dhulma na akalingania katika uadilifu na mapenzi na kushikamana na kusaidiana katika kheri.

- Amelingania katika kusaidia wenye kuhitaji na kutembelea wagonjwa na kupendana na kunasihiana baina ya watu wote.

- Amekataza waislamu matendo maovu kama wizi na ghishi na uuwaji na dhulma.

- Yeye ndo amebadilisha maisha yetu na tabia zetu mbaya kuja katika (tabia) nzuri.

- (Amemfundisha) musilam asiibe.

- (Amemfundisha) muislam asidanganye.

- (Amemfundisha) muislam asinywe pombe.

## Ni nani Mtume Muhammad ﷺ na kitu gani ametufundisha?

- Amemfundisha muislam asizini.

- Amemfundisha muislamu asifanye ghishi.

- (Amemfundisha) musilam asiue wasiokuwa na hatia.

-Amemfundisha muislam asimuudhi jirani yake awe muislam au kafiri.

- Amemfundisha muislam kuwafanyia wema wazazi wake na awahudumie hata kama watakuwa si katika dini yake.

- Amemfundisha muislam kuwaonea huruma watoto na wanawake na wanyonge na watu wazima.

- Amemfundisha muislam asiadhibu watu wala wanyama wala asiharibu mazingira.

## Ni nani Mtume Muhammad ﷺ na kitu gani ametufundisha?

- Amemfundisha muislam amuhurumie na kumpenda mke wake na awatilie umuhimu na kuwaonea huruma watoto zake mpaka siku ya mwisho ya umri wake.

- Amemfundisha muislam asikate mahusiano na watoto wake kwa kufikia watoto wake umri wa balehe.

- Kila muislamu anampenda Muhammad ﷺ kuliko viumbe vyote.

- Amebashir ujio wake Musa na Issa juu yao amani.

- Kila muislam (anampenda) musa na isa na anaamini ya kwamba wao ni katika mitume bora juu yao amani.

- Ametumwa Muhammad ﷺ kwa waarabu na wasio kuwa waarabu.

## Ni nani Mtume Muhammad ﷺ na kitu gani ametufundisha?

- Na hakuna tofauti katika dini yake baina ya mwarabu na asiekuwa mwarabu isipokuwa kwa uchamungu.

- Hakika yeye ni Muhammadﷺ mtume wa Allah .

- Je mmetambua kwa kwa nini waislamu  wote wanampenda Muhammad ﷺ?

- (Je mumejua Muhammad ni nani kwa waislamu?)

Kwa ziada ya elimu kuh usu Mtume Muhammad ﷺ na mafunzo yake...

Website ya sheikh

sarhaan.com

Maahad ya sunna

mahadsunnah.com